# EE SAYUNI UMTUKUZE

Fr. S. Mbunga
Harmonized by Shanel Komba
June, 2026 Dodoma

**Mabeti**




**Kiitikio**







2.a) Nia yetu ya kusifu, Hasa mkate mtakatifu, uletao uzima/
b) Lisho hili walipewa, Wale kumi na wawili, Karamuni mwa mwisho.

3.a) Shangilio la rohoni, Lipendeze liwe zuri, Sifa tele livume/
b) Ipo leo siku kubwa, Kwa kumbusho la kuwekwa, Kwanza ile karamu.

4.a) Muda ule umekwisha, Ipo meza ya Mufalme, Na sheria mpya/
b) Tumepata mapya yote, Nuru siyo nusu giza, Mwanga siyo usiku.

5.a) Tendo lake karamuni, Kristu ametuamuru, Tutende tumkumbuke/
b) Twafuata amri yake, Tukiona hii sadaka, Kwa mkate na divai.

6.a) Mkate wageuka mwili, na divai ikawa damu, Kanuni kwa wakristo/
b) Huelewi huioni, Kweli hiyo ukubali, Maana ni mwujiza mkuu.

7.a) Unaona tu maumbo, Ni alama zifumbazo, Utukufu wenyewe/
b) Ule mwili unywe damu, Kila umbo linamfumba, Yesu mzima halisi.